# OFISI YA MAKAMU WA RAIS
## WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

NA. 00000394

TOLEO MAALUMU - MKUTANO WA COP28, DESEMBA 2023


COP28 UAE




# RAIS SAMIA: TANZANIA INAHAMASISHA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA


*Jarida hili limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania*

Ofisi ya Makamu wa Rais blog.vpo.go.tz

www.vpo.go.tz




## Bodi ya Uhariri

Sigsbert Kavishe
Paul Masanja
Paulo Laiser
Mugisha Kyamani
Ismail Ngayonga
Joyce Mnunguli
Daniel Sagata
Zanipha Msangi

**Limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Ofisi ya Makamu wa Rais**
S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 266 235 2038
Nukushi +266 235 0002
Barua pepe: km@vpo.go.tz
Tovuti: www.vpo.go.tz

Ofisi ya Makamu wa Rais
blog.vpo.go.tz

# Tahariri

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshiriki katika Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) tarehe 30 Novemba- 12 Desemba, 2023. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kauli Mbiu ya Mkutano huo ilikuwa *"Act, Unite and Deliver"*. Kauli mbiu hii inazitaka Nchi Wanachama kutekeleza kwa pamoja Sera, Mipango na Mikakati ya Mabadiliko ya Tabianchi.

Aidha, Kaulimbiu ya Kitaifa ilikuwa ***"Kuimarisha Hatua za Kilimo Himilivu na Uchumi wa Buluu"***. Kauli Mbiu hii ililenga kuchochea hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa na kilimo endelevu na kutumia vizuri fursa za uchumi wa buluu.

Agenda zilizojadiliwa katika mkutano wa COP28 ni pamoja na; Lengo la dunia la Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi; Tathmini ya Kidunia ya Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris; Utekelezaji wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi na Mipango ya Taifa ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi; Hatua wezeshi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; Upatikanaji wa rasilimali fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; Uendeshaji na uwezeshaji wa Mfuko wa hasara na uharibifu unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kuanza kufanya kazi.

Aidha agenda nyingine za Mkutano huo ni Mfumo wa masoko na usio wa masoko wa biashara ya kaboni; Utekelezaji wa Programu ya Sharm El Sheikh kuhusu kilimo na mabadiliko ya tabianchi; Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi; Kuimarisha utekelezaji wa hatua za kupunguza uzalishaji wa gesijoto;

Vilevile, Mkutano huo ulikuwa na Agenda ya Utekelezaji wa Ibara ya Sita ya Makubaliano ya Paris kuhusu Mfumo wa Masoko na usio wa masoko katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; Mfumo wa uwazi katika mikakati na misaada inayotolewa; Uendelezaji na uhaulishaji wa teknolojia na athari za hatua za Sera za Kitaifa na kimataifa.

Katika kuhakikisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inashiriki kikamilifu katika Mkutano huo, Ofisi ya Makamu wa Rais iliratibu na kuandaa Msimamo wa Taifa ambao ulisaidia kuongoza dira ya ushiriki na majadiliano ya wajumbe wa Tanzania katika mkutano wa COP28.

Msimamo huo uliandaliwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Wadau wa Maendeleo, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia kwa kuzingatia Sera, Mipango, Mikakati na Programu za Kitaifa.

Aidha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki mikutano ya Pembezoni na Uwili iliyofanyika sambamba na COP28. Mikutano ya pembezoni ya ngazi ya juu iliyoendeshwa na Tanzania ilihusu; Uzinduzi wa Mpango wa Kukuza Matumizi na Nishati Safi na Nafuu ya Kupikia kwa Wanawake Barani Afrika; na Fursa za uwekezaji kwenye sekta ya kilimo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Mikutano hii iliongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kupitia Mkutano huo Serikali ya Muungano wa Tanzania itanufaika zaidi na fedha za miradi, teknolojia, utaalamu na Programu mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo Programu ya Afrika ya Nishati Safi ya Kupikia; Programu ya Afya na mabadiliko ya tabianchi; na utekelezaji wa mikakati ya kuimarisha uhimili katika sekta ya maji, misitu na Bahari.

Aidha, Matokeo ya Mikutano ya Pembezoni ni Uendeshaji wa Mfuko wa Upotevu na Uharibifu Utokanao na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi, Tathmini ya Kidunia ya Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris, Mpango wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi, Lengo la pamoja la kukusanya fedha za mabadiliko ya tabianchi na Kilimo na Mabadiliko ya Tabianchi.

***#KaziIendelee***

# Yaliyomo




Msimamo wa Tanzania katika Mkutano wa COP28 Uk. 4




Dkt. Jafo aishukuru UNOPS kuisaidia Tanzania miradi ya mabadiliko ya tabianchi Uk. 7



Waziri Jafo akabidhi Tuzo ya Wanawake katika Uongozi kwa mwanamke mfugaji Mtanzania Uk. 10



'Serikali imewawekea Diaspora mazingira mazuri ya kazi' Uk. 14




Rais Samia ahimiza upatikanaji fedha miradi mabadiliko tabianchi Uk. 5



Waziri Makamba: Tanzania itaimarisha ushirikiano na Urenoa Uk. 19




Tanzania kunufaika na Dola milioni 1 kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi Uk. 9

# MSIMAMO WA TANZANIA KATIKA MKUTANO WA COP28




Tanzania inaunga mkono hoja ya kuongeza fedha za ufadhili kwa kuzingatia athari zinazozidi kuongezeka kwa sasa na kuhakikisha ahadi ya nchi zilizoendelea kutoa dola bilioni 100 kila mwaka kwa nchi zinazoendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zinatimizwa.

Kuhakikisha mkutano unaridhia uanzishwaji wa mfuko wa kupambana na majanga na maafa yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi.

Kuhakikisha juhudi za kuelekea matumizi ya nishati safi zinakuwa jumuishi na kujikita pia katika nishati safi za kupikia kwa akinamama vijijini kama njia ya kuhimizia nishati za mpito zinazozingatia usawa wa kijinsia.

Kuhakikisha mjadala wa masuala ya jinsia unaozingatia maadili ya kitaifa na kijamii na wanawake wanapewa kipaumbele katika hatua za kushughulikia mabadiliko ya tabianchi.

COP28 UAE




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza kwenye Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai katika Falme za Kiarabu Desemba 01, 2023.*

# Rais Samia ahimiza upatikanaji fedha miradi mabadiliko tabianchi

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amehimiza mataifa yaliyoendelea kufanikisha upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuongeza kasi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Rais Samia ametoa tamko hilo Desemba 01, 2023 katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Amesema awali ilitolewa ahadi ya dola za Kimarekani bilioni 100 kila mwaka kwa nchi zinazoendelea ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika mkutano wa Copenhagen na ahadi hiyo haijatekelezwa licha ya kiasi hicho kuwa kidogo kuliko kilichohitajika.

Kwa upande mwingine, Rais Samia amesema mkutano wa Paris na Ufaransa iliazimiwa kudhibiti ongezeko la joto chini ya nyuzi joto 1.5, lakini hali ni kinyume kwani kasi ya ongezeko la joto kwa sasa duniani imezidi kuongezeka.

Rais Samia pia amesema kushindwa kutimizwa kwa ahadi hizo kunapunguza mshikamano kwa nchi zinazoendelea, ikiwemo Tanzania ambayo hupoteza kati ya asilimia 2 hadi 3 ya Pato la la Taifa (GDP) kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Akisisitiza kwenye mkutano huo, Rais Samia amesema Tanzania ina nia ya kuhamasisha kuongezwa matumizi ya nishati safi na gharama nafuu ya kupikia na teknolojia kote barani Afrika, hasa kwa wanawake.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wakati wakishiriki moja ya Mikutano kando ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu, Desemba 01, 2023.*

COP28 UAE



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali kabla ya kuzindua Mradi wa Nishati Safi ya kupikia itakayowasaidia Wanawake Barani Afrika (AWCCSP), katika mkutano uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) tarehe 02 Desemba, 2023. Rais Samia alizindua Mradi huo kando ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28).*

# Rais Dkt. Samia azindua Programu ya Nishati Safi ya Kupikia

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameongoza Mkutano wa Pembezoni wa Nishati Safi ya Kupikia wakati wa Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) Desemba 2, 2023.

Katika Mkutano huo Rais Dkt. Samia aliwaongoza viongozi wenzake kutoka nchi mbalimbali duniani na taasisi za kimataifa kuzindua Programu ya Kuwakomboa Wanawake wa Afrika Kupitia Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (African Women Clean Cooking Support Programme - AWCCSP).

Programu hiyo inalenga kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kukabiliana na changamoto za afya, mazingira, uchumi na kijamii ambazo huathiri zaidi wanawake na watoto.

Hali kadhalika, Mheshimiwa Rais alishiriki katika mikutano ya uwili na viongozi wa serikali za nchi mbalimbali pamoja na mashirika ya kimataifa kwa lengo la kuimarisha mahusiano baina ya Tanzania na nchi hizo pamoja na mashirika husika.

Aidha, Rais Dkt. Samia aongoza Mkutano mwingine wa pembezoni uliohusu ***"Accelerating Climate Smart Innovation in Agriculture, addressing Loss Damage and Innovative Sources of Finance"*** uliofanyika Desemba 03, 2023.

Mkutano huo ulilenga katika kuongeza kasi ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi kupitia ubunifu katika sekta ya kilimo na kushughulikia hasara na uharibifu unaotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiangalia video fupi kuhusu matumizi ya Nishati ya kupikia kabla ya kuzindua Mradi wa Nishati Safi ya kupikia itakayowasaidia Wanawake Barani Afrika (AWCCSP), tarehe 02 Desemba, 2023. Rais Samia alizindua Mradi huo kando ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28).*

# Dkt. Jafo aishukuru UNOPS kuisaidia Tanzania miradi ya mabadiliko ya tabianchi

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo ameishukuru Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Huduma za Miradi (UNOPS) kuisaidia Tanzania katika miradi ya mabadiliko ya tabianchi.

Ametoa shukrani hizo wakati wa Mkutano wa Uwili uliofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu Desemba 4, 2023.

Katika mazungumzo hayo, Ujumbe wa UNOPS ulioongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Bw. Jorge Moreira da Silva, Dkt. Jafo ametoa wito kwa taasisi hiyo kuendelea kusaidia miradi hiyo hususan eneo la ujenzi wa kuta katika kingo za bahari na mito.

Hali kadhalika, amechagiza uwezekano wa kupata fedha za miradi ya ujenzi wa mabwawa ya kunyweshea mifugo katika maeneo ya ufugaji ili kuepusha migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Akiendelea kuzungumza katika mkutano huo Waziri Dkt. Jafo ameweka bayana maeneo ya vipaumbele zikiwemo nyanda kame zinazoathiriwa na ukosefu wa maji kwa wakulima na wafugaji.

Kwa upande mwingine viongozi hao wamekubaliana kuendelea kushirikiana katika kushughulikia miradi ya kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Vile vile Waziri Jafo kupitia Serikali na Bw. Da Silva kupitia UNOPS wamekubaliana kwamba taasisi hiyo itasadia katika kuchagiza upatikanaji wa fedha kwa wakati za miradi ya maji na umeme zinazotolewa na Benki ya Dunia (WB).




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Huduma za Miradi (UNOPS) Bw. Jorge Moreira da Silva mara baada ya Mkutano wa Uwili uliofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu Desemba 4, 2023.*

COP28 UAE




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Watanzania mbalimbali wakati alipotembelea Banda la Maonesho la Tanzania, Dubai kwenye Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) Desemba 02, 2023.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai katika Falme za Kiarabu Desemba 01, 2023. Nyuma kushoto ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo, Mshauri wa Rais, Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira, Dkt. Richard Muyungi na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Januari Makamba.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Vijana wanaojishughulisha na masuala ya Mazingira (Green Samia) wakati alipotembelea Banda la Maonesho la Tanzania kwenye viwanja vya Expo Dubai wakati wa Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) Desemba 02, 2023.*

COP28 UAE

# Tanzania kunufaika na Dola milioni 1 kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi

Tanzania inatarajiwa kunufaika na fursa za fedha kiasi cha Dola za Marekani 1,160,000 kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa Mchango wa Taifa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Hayo yamebainishwa wakati wa kikao baina ya Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga na Mkurugenzi wa NDC Partnership, Bw. Pablo Vieira.

Aidha, katika kikao hicho viongozi hao walijadili namna Serikali ya Tanzania inaweza kupata miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi..

Maeneo mengine yaliyojadiliwa ni namna ya kuiwezesha Tanzania kupata fedha za kujenga utayari wa nchi kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na upatikanaji wa Ithibati kwa Taasisi za Tanzania ili kuweza kupata fedha za kukabiliana ana Mabadiliko ya Tabianchi.

Katika hatua nyingine, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri alitoa taarifa ya utekelezaji wa Mradi wa maji wa Simiyu Water Climate Resilience Phase II wenye thamani ya Euro Milioni 144 unaofadhiliwa na GCF.

Mhandisi Mwajuma amesema GCF ilionesha utayari wa kuisaidia Tanzania katika mradi huo wa maji na imeahidi kutuma timu ya wataalamu kufika nchini Tanzania mwaka 2024 kwa ajili ya kukutana na wadau wakiwemo taasisi zinazoomba ithibati.

Kikao hicho pia kilishirikisha wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Raisi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Wizara ya Maji, Wizara ya Fedha, TAMISEMI, Benki za CRDB, NMB na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).




*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (katikati) akiwa katika kikao na Mkurugenzi wa Mashauriano wa Taasisi ya NDC Partnership, Bi Mariana Panuncio wakati wa Mkutano wa pembezoni wa COP28. Kushoto ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Dkt. Omar Dadi Shajak.*

COP28 UAE

# Waziri Jafo akabidhi Tuzo ya Wanawake katika Uongozi kwa mwanamke mfugaji Mtanzania



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akikabidhi Tuzo ya 'Wanawake katika Uongozi' kwa Baraza la Wanawake Wafugaji (PWC) Tanzania, mshindi wa kwanza kati ya washindani 500 duniani wa tuzo iliyotolewa na Taasisi ya Global Centre on Adaptation (GCA) kwa Kiongozi wa Baraza hilo kutoka jamii ya Kimasai Bi. Maanda Ngoitiko, Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu ambako ulifanyika Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28).*




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiwa katika picha ya pamoja na Watanzania wanaoshiriki Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) jijini Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu mara baada ya kukabidhi Tuzo ya 'Wanawake katika Uongozi' kwa Baraza la Wanawake Wafugaji (PWC) kupitia kwa Kiongozi wake Bi. Maanda Ngoitiko (wa pili kushoto).*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amekabidhi Tuzo ya 'Wanawake katika Uongozi' kwa Baraza la Wanawake Wafugaji (PWC) Tanzania baada ya kuibuka mshindi wa kwanza kati ya washindani 500 kutoka nchi mbalimbali duniani.

Tuzo hiyo imetolewa na Taasisi ya Global Centre on Adaptation (GCA) jijini Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu ambako Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) umefanyika.

Akikabidhi tuzo hiyo kwa Kiongozi wa Baraza hilo kutoka jamii ya Kimasai Bi. Maanda Ngoitiko aliyeipokea kwa niaba ya Baraza hilo, Dkt. Jafo amewapongeza kwa kuipatia Tanzania sifa.

"PWC wameiheshimisha sana Tanzania na kuifanya isikike duniani na nina uhakika kabisa tuzo hii imetokana na juhudi binafsi za dada yangu Maanda za kuimarisha uwezo wa uongozi wa wanawake wafugaji kwa kuwajengea uwezo kiasi cha kufikia usawa katika kutoa maamuzi katika jamii zao," amesema Waziri Jafo.

Akishukuru kwa tuzo hiyo Bi. Maanda amesema kuwa Baraza hilo linawahudumia wanawake na wasichana kutoka jamii za Wamasai, Sonjo, Akie na Barabaig.

Amesema, PWC ni shirika lisilo la kiserikali linalofanya kazi kaskazini mwa Tanzania kufikia usawa wa kijinsia na maendeleo ya jamii kupitia uwezeshaji wa wanawake na wasichana wa Kimasai.

COP28 UAE



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis akizungumza na Mshauri wa Rais, Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira Dkt. Richard Muyungi alipowasili katika banda la Tanzania, viwanja vya Expo City, Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).*



*Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis (kushoto) akitembelea banda la Tanzania katika viwanja vya Expo City Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Wengine wa pili kulia ni Afisa Mazingira Mwandamizi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Mwanaasha Tumbo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Sarah Kibonde.*




*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mshauri wa Rais, Masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi Dkt. Richard Muyungi (wa pili kushoto) na wawakilishi wa vijana, kundi la Green Samia, wakiwa nje ya banda la Tanzania, viwanja vya Expo City Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).*

# Dkt. Jafo: Serikali imeimarisha huduma za hali ya hewa kupitia teknolojia

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amesema Serikali imeweka kipaumbele katika kuimarisha huduma za hali ya hewa na mifumo ya tahadhari ya mapema kupitia Mifumo, Sera na Teknolojia.



Amesema hayo wakati akizungumza kwenye Jukwaa la Mawaziri la Majadiliano ya Juu la Utekelezaji wa Tahadhari ya Mapema kwa Wote katika Mpango Kazi wa Afrika lililofanyika pembeni ya Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu.

Dkt. Jafo amesema Serikali inahakikisha inapunguza athari za majanga kwa kuboresha ustawi na uthabiti wa watu wake na jamii kama sehemu ya mkakati wa maendeleo kwani majanga ni matokeo ya maafa yanayoathiri mipango na malengo ya maendeleo yake.

"Ni muhimu kujiandaa kupitia mifumo ya tahadhari ya mapema kwani inaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa athari na kuokoa maisha ya watu na mali nyingi na kwa umuhimu huo Tanzania imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021-2026) pamoja na Mchango wa Kitaifa wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (NDC)," amesema.

Aidha, Waziri Jafo amesema kuwa Serikali ya Tanzania ilitunga Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya mwaka 2019, inayotoa maelekezo na kuimarisha Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kutoa Huduma za Tahadhari za Mapema.

Ameongeza kuwa Serikali pia ilikuja na Mifumo ya Kitaifa ya Huduma za Hali ya Hewa (NFCS), ambayo ilizinduliwa Agosti 2018 sanjari na kufunga rada saba za hali ya hewa na tayari zimeanza kufanya kazi.

Hata hivyo, Dkt. Jafo amesema imeanzishwa shahada katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhusu masuala ya Hali ya Hewa na Mabadiliko ya Tabianchi, kusaidia kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu nchini hasa kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Kutokana na taarifa za hali ya hewa kutoka TMA, amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Wadau wote wenye dhamana iliandaa Mpango wa Taifa wa Dharura wa El Nino na hatua ya matarajio Agosti, 2023 ambao umechangia kupunguza athari za mvua hizo.

"Nachukua fursa hii kuthibitisha dhamira ya Tanzania ya kufanya kazi na WMO, wadau, na Wanachama wengine wa WMO katika kuboresha uwezo wa Mamlaka zetu za Hali ya Hewa kwa manufaa ya watu wetu na mataifa yetu," amesema Dkt. Jafo huku akibainisha kuwa TMA inatoa usahihi wa utabiri wa hali ya hewa kwa zaidi ya asilimia 86.

Hivyo amesema, TMA inaboresha uwezo wa kufanya kazi kwa watumishi wake ambapo asilimia 14.5 wamepewa ujuzi na maarifa juu ya programu za hadhari katika taasisi mbalimbali za mafunzo ndani na nje ya Tanzania.

COP28 UAE



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (wa pili kulia) akiwa nje ya banda la Tanzania - katika Viwanja vya Dubai Expo City Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE) Desemba 02, 2023. Wengine Kuanzia kushoto ni Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Prof. Riziki Shemdoe, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Bi. Amina Khamis Shaaban, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Dkt. Omar Dadi Shajak na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Felchesmi Mramba.*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais walioshiriki Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (kulia) akiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Felchesmi Mramba wakiwa katika Viwanja vya Dubai Expo wakati wa Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) ulioanza Novemba 30 hadi Desemba 12, 2023.*

COP28 UAE

# 'Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa Diaspora'

Serikali imesema inatambua mchango na umuhimu wa Watanzania waishio nje ya nchi (Diaspora) katika kuleta maendeleo nchini Tanzania.

Hayo yamesemwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hotuba yake iliyosomwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo (pichani) wakati wa Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara (Siku ya Mtanzania) yaliyofanyika Desemba 9, 2023 Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Amesema tayari Serikali imechukua hatua ya kusaini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano kwenye kazi na ajira uliosainiwa katika kipindi cha Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28).

Hivyo, amesema hatua hiyo itasaidia katika kutatua changamoto nyingi zilizokuwepo za wafanyakazi hasa wa majumbani na wote kwa ujumla watakuwa katika mazingira mazuri ya kisheria kwa pande zote mbili.



Waziri Jafo amesema hatua hizo za makusudi ni mojawapo ya mikakati ya Serikali katika kuhakikisha Diaspora wanawekewa mazingira wezeshi ya kuwatambua kisera na kisheria. Dkt. Jafo amesema kuwa Rasimu ya Sera ya Mambo ya Nje iko katika hatua za mwisho chini ya uratibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo imewatambua.

Amesema katika Sera hiyo mpya kutakuwa na kipengele maalumu cha Diaspora ambapo Serikali imeanza na mkakati ya kuwawekea hadhi maalumu Watanzania hao.

"Ni mategemeo ya Serikali kuwa Diaspora mtakuwa na upendeleo maalumu ikiwa ni pamoja na kuweza kurudi Tanzania kirahisi na kuweza kunufaika na fursa mbalimbali za kichumi tofauti na wageni kwani katika kipindi chote cha historia, uhusiano kati ya Tanzania na UAE umekuwa wa kipekee," amesema Dkt. Jafo.

Aidha, Dkt. Jafo ameongeza kuwa yapo mafanikio mengi yakiwemo ushirikiano wa kibiashara, utamaduni na maendeleo ya kijamii na ili kuendelea kunufaika na fursa zilizopo katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu kwa kupitia uhusiano mzuri uliopo kati ya nchi hizi mbili.

Kwa upande mwingine amesema Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imezindua mfumo wa mawasiliano na Diaspora wake kote duniani uitwao Diaspora Digital Hub System (DDH) ambao utasaidia usajili wa wanadiaspora wa makundi yote kwa lengo la kuwatambua na kuwaweka katika mfumo maalumu ili iwe rahisi kwa mawasiliano na kuwaunganisha katika mitandao ya huduma muhimu.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiwa na Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) Mhe. Luteni Jenerali (Mstaafu) Yacoub Hassan Mohamed wakati wa Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara (Siku ya Mtanzania) yaliyofanyika Desemba 9, 2023 Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).*

COP28 UAE



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akizungumza na wadau mbalimbali katika banda la Tanzania katika Viwanja vya Dubai Expo City, Dubai - Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akizungumza na Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Kemilembe Mutasa katika banda la Tanzania katika Viwanja vya Dubai Expo City, Dubai - Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiteta jambo na Afisa Mazingira Mwandamizi Ofisi ya Makamu wa Rais Mhandisi Bi. Mwanaasha Tumbo katika banda la Tanzania -B86 lililopo katika Viwanja vya Dubai Expo City, Dubai - Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).*

COP28 UAE

*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga akizungumza na wageni mbalimbali waliotembelea banda la Tanzania - Viwanja vya Dubai Expo City, Dubai - Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Dkt. Omar Dadi Shajak (wa pili kulia) na wataalamu kutoka Tanzania Zanzibar katika banda la Tanzania - Viwanja vya Dubai Expo City, Dubai - Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).*




*Washiriki wa Tanzania wakiwa katika banda la Maonesho la Tanzania, Viwanja vya Dubai Expo City, Dubai – Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) .*



COP28 UAE






*Wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais wakitoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali kwa wananchi waliotembelea banda la Tanzania - B86 katika Viwanja vya Dubai Expo City, Dubai - Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE)*





# Mkutano wa COP28 wafungua milango sekta ya kilimo

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imepata mafanikio makubwa ya uwezeshaji na uwekezaji mkubwa kupitia mikutano ya pembezoni na uwili ya Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliomalizika tarehe 12 Desemba, 2023 Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu.

Katika Mikutano ya pembezoni na Uwili, Viongozi wa Serikali waliongozwa na Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Kilimo, Mhe. Waziri Hussein Bashe na Watendaji Waandamizi wa Wizara ya kilimo waliweza kushiriki katika Mikutano mbalimbali na wadau wa maendeleo iliyolenga kukuongeza chachu ya uwekezaji na uwezeshaji katika Sekta ya Kilimo ili kuvutia Wawekezaji

Miongoni mwa Mkutano ya awali ni ni Mkutano wa Agricultural Opportunities for Green Growth Transformation in Tanzania ambao ulihudhuriwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ukiwa na lengo la kukusanya kiasi cha Dola za Kimarekani 1.8 Bilioni kwa ajili ya kuchimba visima 65,000 vyenye uwezo wa kuhudumia wakulima 16 wenye mashamba ya ukubwa wa hekta 2.5.

Kupitia Mkutano huo, wadau waliahidi kuichangia Serikali ya Tanzania kiasi cha Dola za kimarekani Milioni 610, ambapo Benki ya Dunia (WB) iliahidi kuchangia Dola Milioni 300, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Dola Milioni 100, Shirika la Ukuzaji endelevu wa mifumo ya chakula Afrika (AGRA) Dola Milioni 50, Shirika la Maendeleo ya Kilimo Ulimwenguni (IFAD) Dola Milioni 60 na Shirika la Misaadala Marekani (USAID) Dola Milioni 100.

Aidha katika Mkutano mwingine Wizara ilishirikiana na Taasisi za Kimataifa katika kuandaa mkakati wa pamoja wa Kuongeza Kasi ya Kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi Katika Sekta ya Kilimo kwa Kushughulikia hasara na uharibifu unaotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi l.

Mkutano mwingine uliohusisha Wizara ya Kilimo ni pamoja na Azimio la pamoja la kuendeleza Kilimo Endelevu na kuimarisha Mifumo ya chakula katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi, ambapo Mkakati huu wa pamoja wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi una lengo la kuweka nguvu ya pamoja katika kutafuta rasilimali fedha za kilimo na mabadiliko ya tabianchi duniani.

Manufaa mengine yaliyopatikana katika azimio hilo ni pamoja na kuwezesha maandiko ya vipaumbele vya miradi ya sekta ya kilimo katika upatikanaji wa ufadhili na kuongeza chachu ya uwekezaji katika masuala ya uhimilivu wa mifumo ya chakula na kuimarisha uchumi wa kijani.

Aidha Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe aliweza kufanya mikutano ya uwili na wadau wa maendeleo akiwemo Makamu wa Rais Benki ya Maendeleo Afrika, Dkt. Beth Dunford.

Kauli Mbiu ya Mkutano wa COP28 ilikuwa "Unite, Act, Deliver" ikilenga kuzitaka Nchi Wanachama wa Mkataba kuungana, kutekeleza na kuleta matokeo ya pamoja katika sera, mipango na mikakati ya mabadiliko ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

# Dkt. Nchemba: Tanzania kukamilisha mfumo endelevu wa uchambuzi wa takwimu za fedha za miradi



Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba amesema Tanzania itaendelea kushirikiana na Benki ya Standard Chartered katika kusimamia ukamilishaji wa mfumo endelevu wa uchambuzi wa takwimu za matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo.

Dkt. Nchemba amesema hayo wakati wa Mkutano wake na Mkurugenzi wa Benki ya Standard Chartered Bank, Bw. Salman Ansari uliojadili Mfumo Endelevu wa Ugharimiaji Fedha katika miradi ya Mabadiliko ya Tabianchi na miradi ya jamii pembezoni mwa Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) Dubai- Umoja wa Falme za Kiarabu.

Kwa mujibu wa Waziri Nchemba amesema Tanzania imekuwa na ushirikiano wa muda mzuri na Benki ya Standard Chartered katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya mabadiliko ya tabianchi.

Aidha Dkt. Nchemba amesema Benki ya Standard Standard ni miongoni washirika wa maendeleo wa Tanzania wanaochangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nguzo za maendeleo ya benki, uwekezaji wa fedha katika miradi endelevu na ujumuishaji.

Waziri Nchemba amefafanua kuwa Benki ya Standard Chartered imekuwa ikiunga mkono juhudi za Serikali na Jumuiya ya Kimataifa katika kuimarisha ustawi wa jamii na kulinda mazingira kwa ustawi wa vizazi vya sasa na vijavyo.

"Mkutano huu umejikita katika majadiliano ambayo yatawezesha kuandaa maandalizi ya upatikanaji wa fedha za kugharimia miradi ya mabadiliko ya tabianchi kwa mfumo wa hatifungani na mbinu endelevu za kuchochea maendeleo" amesema Dkt. Nchemba.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Benki ya Standard Chartered Bw.....amesema Mabadiliko ya Tabianchi ni ajenda inayoendelea kujadiliwa katika majukwaa na mikutano mbalimbali ya kidunia kwa sasa kutokana na matukio makubwa yanayoendelea kutokea ikiwemo mvua, mafuriko na ongezeko la joto.

"Standard Chartered inachukulia Mabadiliko ya Tabianchi kama mojawapo ya changamoto kubwa zaidi za kimazingira zinazoukabili ulimwengu, ikizingatiwa athari zake zilizoenea na kuleta athari kwa afya ya binadamu na ukuaji wa uchumi" amesema.

Aidha amefafanua kuwa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia, Benki hiyo imeendelea kutoa fedha katika Nchi zinazoendelea ili kuanzisha na kutekeleza miradi ya uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.




# Waziri Makamba: Tanzania itaimarisha ushirikiano na Ureno

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. January Makamba amesema inakamilisha mashauriano ya mifumo ya kisera na kisheria ili kuhakikisha Mkataba wa Makubaliano (MoU) katika sekta ya uwekezaji baina ya Serikali ya Ureno na Tanzania unasainiwa.

Waziri Makamba aliyasema hayo Desemba 2, 2023 wakati wa Mkutano wa pembezoni na Waziri wa Mambo ya Nje wa Ureno, Mhe. Gomes Cravinho katika Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko Mkutano wa (COP 28) uliofanyika Dubai- Umoja wa Falme za Kiarabu Novemba 28- Desemba 12, 2023.

Mhe. Makamba amesema alimkaribisha Waziri Cravinho kufanya ziara nchini Tanzania mwanzoni mwa mwaka 2024, itakayotoa fursa ya kukamilisha Hati ya Makubaliano (MOU) husika na kuimarisha ushirikiano wa uwili uliopo baina ya Tanzania na Portugal.

Waziri Makamba amesema Tanzania imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama inaendelea kuimarisha katika Ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na kutolea mfano uwepo wa Askari wa Kulinda Amani wa Tanzania katika eneo la Cabo Delgado nchini Msumbiji.

Kwa upande wake Waziri wa Mambo ya Nje wa Ureno Mhe. Gomes Cravinho amesema utiaji saini wa Mkataba wa Makubaliano (MoU) baina ya Ureno na Taasisi za Uwekezaji katika sekta za biashara za Tanzania ikiwemo Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Kuendeleza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) utasaidia kuimarisha kwa sekta ya usafirishaji nchini.

Mhe. Cravinho amesema kuwa katika Mkutano wa COP 28 mwaka 2023, Serikali ya Ureno ilifanya mkutano na Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu masuala ya fedha na Mabadiliko ya Tabianchi na Tanzania inatarajia kunufaika na fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Aidha Mhe. Cravinho aliwasilisha ombi kwa Serikali ya Tanzania kuiunga mkono Ureno katika kugombea nafasi ya mjumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa mwaka 2027/2028 katika uchaguzi utakaofanyika mwaka 2026.

Akitoa mrejesho wa suala hilo, Mhe. Waziri Makamba alieleza kuwa Tanzania itaiunga mkono Ureno katika nafasi hiyo na kueleza kuwa itawasilisha mawasiliano hayo rasmi kupitia Waraka wa Kidiplomasia.



# IUCN kuipatia Tanzania bilioni 76 kukabili mabadiliko tabianchi

Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira (IUCN) inatarajia kuipatia Tanzania kiasi cha Shilingi Bilioni 76 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Barani Afrika ujulikanao Blue Green Wall (BGW).

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Kanda ya Kusini na Mashariki ya Afrika wa IUCN, Luther Bois Anukur wakati wa Mkutano wa pembezoni na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulega katika Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) uliomalizika hivi karibuni Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Waziri Ulega amesema Mradi huo umekusudia kuboresha kosaafu za mifugo kwa mikoa ya Singida na Manyara ambao umelenga kuhakikisha wafugaji wanazingatia uhifadhi na utunzaji wa mazingira sambamba na ili kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai na mazao mengine ya mifugo.

Ameongeza kuwa mradi huo pia umelenga kuhimiza matumizi ya teknolojia na matokeo ya tafiti mbalimbali zitakazosaidia uhifadhi na utunzaji wa mazingira ikiwemo ili kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi na hatimaye kuongeza uzalishaji na kuleta tija kwa wafugaji.

Amefafanua kuwa Serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwemo kuanzisha mpango wa mabadiliko ya sekta ya mifugo unaolenga kuwasaidia wafugaji ikiwa ni pamoja na kutambua mabadiliko ya tabianchi na athari zake.

Mhe. Ulega amesema athari za Mabadiliko ya Tabianchi ikiwemo ukame umesababisha wafugaji wengi kutafuta sehemu za malisho, hivyo kupitia Mradi huo Serikali imekusudia kuhakikisha kuwa wafugaji wengi wanafuga kisasa na kunufaika.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa IUCN, Bw. Luther Bois amesema ni wazi kuwa nchi zinazoendelea ikiwemo zile za Afrika zitahitaji msaada kutoka nchi tajiri ili zitekeleze mipango ya kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na hatimaye mifumo ya kilimo na chakula iwe endelevu.

Aidha ameeleza kuwa katika karne hii kumeshuhudia kuongezeka kwa kiwango cha juu cha wastani wa joto, na magonjwa vinatarajiwa kuwa na madhara kwenye uzalishaji wa mazao, mifugo, uvuvi na kilimo cha mazao ya bahari-ni, na hivyo kuhitaji juhudi za pamoja za kuzuia hali hiyo.

“Mabadiliko ya Tabianchi yataathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo, mifugo na sekta ya biashara na kuleta wasiwasi katika usalama wa chakula katika nchi nyingi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara, Aidha katika Mkutano wa COP 28, Waziri Ulega alifanya Mikutano mbalimbali ikiwemo Mkutano na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Dunia, Dkt. Martien Van Niewkoop, Mkutano na Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya WorldFish Dr. Essam Yassin Mohamed pamoja na Mikutano mingine mbalimbali.

# Waziri Aweso akutana na wadau mbalimbali wa sekta ya maji

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso amekutana na kufanya mazungumzo na wadau ikiwemo taasisi na mashirika mbalimbali ya Kimataifa katika Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabianchi uliomalizika mwanzoni mwa Desemba, 2023.

Katika Mkutano huo, Waziri Aweso mbali na mikutano yake na wadau wa kimkakati ikiwemo kikao cha ushirikiano baina ya Benki ya Maendeleo ya Africa (AfDB) pamoja Wizara ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Malawi kuhusu Ujenzi wa Bwawa la Lower Songwe na Mtambo wa Kuzalisha Umeme wa Megawati 180.

Katika kikao kingine, Waziri Aweso alishiriki Mkutano na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) kuhusu ujenzi wa Bwawa la Lugoda katika Mto Ndembera litakalotumika kwa ajili ya Kilimo cha Umwagiliaji hekta 3,600, eneo la Madibira Mkoa wa Iringa.

Mhe. Aweso pia alishiriki kikao na Ofisi ya ya Misaada ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Uingereza-(FCDO) kujadili uwezekano wa nchi ya Tanzania kujiunga na Taasisi ya Glasgow Declaration on Fair Water FootPrints, ambapo Mkataba huo utasainiwa utaiwezesha Tanzania kunufaika na Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Maji utakaogharimu Pauni za Uingereza Millioni 39.

Mhe. Aweso pia alishiriki kikao baina ya Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) uliolenga katika kuhamasisha ushiriki wa Tanzania katika Progamu ya Urban Water Catalyst Initiative katika kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wa Mamlaka za Maji Duniani.

Programu hizo zinafadhiliwa na Serikali za Uholanzi na Ujerumani na kusimamiwa na Shirika ya GIZ na Benki ya KfW zote za Ujerumani.

Kikao kingine na wadau ni pamoja na Kikao na Taasisi ya Global Green Fund (GCF) kilichojadili uwezekano wa kuanza utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Kupeleka Maji Mkoa wa Simiyu inayohusisha Wilaya za Meatu na Maswa.

Waziri Aweso pia alifanya Kikao na Shirika la Mazingira la Dunia (GEF) kilichojadili Miradi Miwili ambayo itawasilishwa kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji. Miradi hiyo ni ya Mabonde ya Ruvuma na Wami Ruvu.







*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akizungumza na waandishi wa habari Desemba 18, 2023 jijini Dar es Salaam kuhusu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu.*

wa ngazi ya juu kuhusu fursa za uwekezaji kwenye sekta ya kilimo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi , mkutano wa kuongeza kasi ya kupambana na mabadiliko ya tabia nchi katika sekta ya kilimo kwa kushughulikia hasara na uharibifu unaotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi ," amesema.

Aidha, Kupitia Mkutano wa COP28 kampuni na taasisi 56 zimeonesha nia ya kuwekeza nchini kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Dkt.Jafo amesema katika mkutano huo sekta binafsi na Asasi za Kiraia (AZAKI) 340 zilishiriki ipasavyo katika mkutano wa COP28 ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB, CRDB, NBC pamoja na NMB) ambazo zilikuwa sehemu kubwa ya wajumbe wa Tanzania walioshiriki katika mkutano huo.

Mkutano wa 29 (COP 29) umepangwa kufanyika nchini Azerbaijan kuanzia Novemba 11 hadi 22, wakati COP30 itafanyika nchini Brazil kuanzia Novemba 10 hadi 21, 2025.

# Mkutano wa COP 28 Dubai waleta neema Tanzania



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo (pichani) amesema Tanzania inatarajia kunufaika na fedha za miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi huku kampuni 56 zikionesha nia ya kuwekeza nchini.

Ametoa kauli hiyo Desemba 18, 2023 jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu.

Dkt. Jafo amesema kupitia mikutano ya pembezoni iliyohusisha majadiliano kati ya Tanzania na wadau kutoka nchi mbalimbali, uliofanyika Novemba 30 hadi Desemba 12, 2023 Tanzania itanufaika na teknolojia na Programu ya Afrika ya Nishati Safi ya Kupikia pamoja na afya.

Amesema kuwa programu hiyo inaunga mkono juhudi za Serikali za kuhamasisha kuachana na matumizi ya kuni na mkaa ambayo yanasababishwa na ukataji wa miti.

Pamoja na manufaa hayo, Waziri Jafo amesema kuwa utekelezaji wa mikakati ya kuimarisha uhimili katika sekta ya maji, misitu na bahari ambayo ni mojawapo ya rasilimali muhimu kwa uchumi wa buluu.

"Mkutano huo umekuwa na mafanikio kwani tumejadili fursa za uwekezaji kwenye sekta ya kilimo katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hivyo kuongeza kasi ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

"Tumejadili mikakati ya kukusanya Dola za Marekani bilioni 1.8 kwa ajili ya kuchimba visima 65,000 ambapo kila kisima kimoja kitahudumia wakulima wenye mashamba ya ukubwa wa hekta 2.5 huku wadau wa maendeleo waliahidi kuchangia programu hii Dola za Marekani milioni 610," amesema huku akiongeza kuwa programu hiyo itasaidia uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya Kilimo na itapunguza uharibifu wa mazingira.

Halikadhalika, amebainisha katika kuwezesha Serikali inashiriki kikamilifu, Tanzania iliandaa msimamo wa nchi uliosaidia kuongoza majadiliano ya wajumbe wa Tanzania na wadau mbalimbali.

Aidha, Dkt. Jafo amebainisha kaulimbiu ya Tanzania ilikuwa ***'Kuimarisha Hatua za Kilimo Himilivu na Uchumi wa Buluu',*** iliyolenga kuchochea hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa na kilimo endelevu na kutumia vizuri fursa za uchumi wa Buluu.

"Pia kulikuwa na mkutano wa ngazi ya juu kuhusu fursa za uwekezaji kwenye sekta ya kilimo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi , mkutano wa kuongeza kasi ya kupambana na mabadiliko ya tabia nchi katika sekta ya kilimo kwa kushughulikia hasara na uharibifu unaotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi ," amesema.

Aidha, Kupitia Mkutano wa COP28 kampuni na taasisi 56 zimeonesha nia ya kuwekeza nchini kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Dkt.Jafo amesema katika mkutano huo sekta binafsi na Asasi za Kiraia (AZAKI) 340 zilishiriki ipasavyo katika mkutano wa COP28 ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB, CRDB, NBC pamoja na NMB) ambazo zilikuwa sehemu kubwa ya wajumbe wa Tanzania walioshiriki katika mkutano huo.

Mkutano wa 29 (COP 29) umepangwa kufanyika nchini Azerbaijan kuanzia Novemba 11 hadi 22, wakati COP30 itafanyika nchini Brazil kuanzia Novemba 10 hadi 21, 2025.

COP28 UAE

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la Tanzania wakati wa Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) ulioanza Novemba 30 hadi Desemba 12, 2023. Kushoto ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akifurahia jambo na washiriki kutoka Tanzania wakati wa Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) alipotembelea banda la Tanzania.




Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (kushoto) akiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira Mhe. Jackson Kiswaga na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi nje ya banda la Tanzania wakati wa Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) alipotembelea banda la Tanzania.



COP28 UAE




*Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe akishiriki mkutano wa pembezoni wakati wa Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) ulioanza Novemba 30 hadi Desemba 12, 2023.*




*Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega akishiriki mkutano wa pembezoni wakati wa Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) ulioanza Novemba 30 hadi Desemba 12, 2023. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Semesi*




*Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Juma Waziri akishiriki mkutano wa pembezoni wakati wa Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) ulioanza Novemba 30 hadi Desemba 12, 2023.*

# Mkutano wa COP28 watoa mwelekeo kukabili mabadiliko tabianchi




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (wa pili kushoto - msiari wa tatu kutoka mbele) akiwa katika picha ya pamoja na Wakuu wa Nchi na Serikali katika ufunguzi wa Mkutano wa COP28 uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kuanzia tarehe 30 Novemba — 12 Desemba, 2023*

Katika mkutano wa majadiliano ngazi ya Wataalamu Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, sekta binafsi na Asasi za Kiraia iliratibu kuwasilisha na kutoa mwongozo wa majadiliano ya kitaalamu kupitia msimamo wa Nchi wa mkutano wa 28 ambao iliandaa.

Masuala muhimu yaliyojadiliwa katika mkutano wa 28 na makubaliano yaliyofikiwa ni kama Lengo la pamoja la kuhimili mabadiliko ya Tabianchi ambapo majadiliano yalilenga kujadiliana rasimu ya andiko la mwongozo wa kuandaa lengo la pamoja la kidunia litakalowezesha nchi zinazoendelea kuhmili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Uamuzi Uliofikiwa ni Nchi wanachama kukubaliana kuhusu Lengo la dunia la Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi pamoja na Mwongozo wake ambao unabainisha mwelekeo ambao jumuiya ya kimataifa inapaswa kutekeleza ili kuwezesha jitihada za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo shabaha za kuwezesha kuhimili mabadiliko ya tabianchi; mahitaji ya rasilmali fedha, teknolojia na kujenga uwezo.

### Uendeshaji wa Mfuko wa Upotevu na Uharibifu Utokanao na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi

Majadiliano yalihusu masuala ya uendeshaji wa mfuko ulioanzishwa wa kukabiliana na upotevu na uharibifu utokanao na athari za mabadiliko ya tabianchi (Loss and Damage Fund) na kuanzishwa kwa Bodi ya Ushauri wa Mfuko. Uamuzi Uliofikiwa ni Uendeshaji wa Mfuko wa kukabiliana na upotevu na uharibifu utokanao na mabadiliko ya tabianchi pamoja na Bodi ya ushauri ya Mfuko huo makubaliano. Nchi wanachama wamekubaliana kuwa Benki ya Dunia itausimamia Mfuko kwa kipindi cha miaka mitano na Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa inashughuhlikia Majanga (UNDRR) itakuwa Sekretarieti ya Bodi ya Ushauri.

Jumla ya Dola za Marekani Milioni 783.98 zimeahidiwa kutolewa kwa ajili Mfuko huo. Nchi ambazo tayari zimetoa ahadi ni Umoja wa Ulaya; Italia; Umoja wa Falme za Kiarabu; Ujerumani; Uingereza; Uholanzi; Marekani; Japan; Norway; Canada; Slovenia; Ufaransa.

### Tathmini ya Kidunia ya Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris

Katika agenda ya tathmini ya kidunia ya makubaliano ya Paris majadiliano yalihusu masuala mbalimbali ya utekelezaji wa Makubaliano ya Paris ikiwemo mwelekeo wa ufikiaji lengo la dunia la upunguzaji wa gesijoto kufikia nyuzi joto 1.5 mwaka 2030, na utekelezaji wa ahadi kwa nchi zilizoendelea wa ukusanyaji fedha kiasi cha Dola za Marekani bilioni 100 ifikapo mwaka 2020 ili kuzisaidia nchi zinazoatharika zaidi na mabadiliko ya tabianchi.

Kulingana na taarifa ya Kamati husika ilibainisha kuwa ufikiaji wa malengo ya Makubaliano ya Paris siyo wa kuridhisha ikiwemo utekelezaji wa ahadi kwa nchi zilizoendelea wa ukusanyaji fedha za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Uamuzi uliofikiwa ni Tathmini ya Kwanza kukamilika na kupitishwa na mchakato wa kuanza tathmini ya pili

umepitishwa. Tathmini hiyo iliangazia masuala ya upunguzaji wa gesijoto ambapo zinahitaji kupunguzwa kwa asilimia 43 ifikapo mwaka 2030 ili kuwezesha joto la dunia kutopanda zaidi ya nyuzi joto 1.5°C.

Baadhi ya hatua ni pamoja na kuongeza matumizi ya nishati jadidifu, kuongeza jitihada za kuachana na matumizi ya nishati chafuzi na kuondoa ruzuku kwa matumizi ya makaa ya mawe; kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na ushirikishwaji wa sekta binafsi na asasi za kiraia.

Aidha, wanachama wametakiwa kupitia Michango yao ya Kukabiliana na Mabadiliko ya tabianchi na kuhuisha matokeo ya tathmini ya kidunia ifikapo mwaka 2025 ambapo NDCs zilizoboreshwa zitaandaliwa na kuwasilishwa Sekretarieti ya Mkataba.

### Mpango wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi

Majadiliano katika Mkutano wa 28 yalilenga kuzisaidia nchi zinazoendelea kuweza kuandaa, kuhuisha na kutekeleza Mipango ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, majadiliano yalihusisha taarifa ya Kamati ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Committee) na Kamati ya Wataalamu ya nchi zinazoendelea (Least Developed Countries Expert Group-LEG) kuhusu mapungufu, mahitaji na taratibu za kuandaa na kutekeleza NAPs.

Majadiliano yalihusu mapendekezo ya kutoa mwongozo kwa Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF) ili uweze kutoa fedha kwa nchi zinazoendelea kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza NAPs pamoja na utekelezaji wa mpangokazi ulioandaliwa na Kamati ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi.

Uamuzi Uliofikiwa ni Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi na nchi wanachama kwa pamoja zimeombwa kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa mpango kazi wa Kamati ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi.

Aidha, Kamati ya Wataalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi na Kamati ya Kuhimili mabadiliko ya Tabianchi zimeombwa kuendelea kutoa miongozo, mafunzo na kuendesha warsha ili kubaini mahitaji ya nchi zinazoendelea katika kuandaa na kutekeleza Mipango ya Taifa ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi. Makubaliano hayajafikiwa, yataendelea katika Mkutano wa 29.

Majadiliano yalihusu taarifa za upatikanaji endelevu wa fedha na usimamizi wa fedha katika mifuko ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Hoja zilizojadiliwa ni pamoja na upatikanaji wa Dola za Marekani bilioni 100 kila mwaka ifikapo mwaka 2025, upatikanaji wa fedha nyingine zilizoahidiwa na nchi zilizoendelea katika mkutano wa 26 na mawanda au maana ya fedha za mabadiliko ya tabianchi.

Mambo mengine yaliyojadiliwa ni pamoja na mfumo wa usimamizi wa Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi, wito wa kuongeza mara mbili fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kama ilivyokubaliwa katika mkutano wa 26 na mchakato wa ithibati kwa taasisi za kitaifa na kikanda katika Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund - GCF).

Uamuzi uliofikiwa ni Kamati ya kudumu ya fedha imeagizwa kuandaa taarifa na muhtasari kuhusu muelekeo wa kufikia lengo la ukusanyanyaji wa Dola za Marekani Bilioni 100 kila mwaka kwa ajili ya kushughulikia mahitaji ya nchi zinazoendelea. Taarifa hii itakuwa inaadaliwa kila baada ya miaka miwili na itaanza mwaka mwaka 2024 hadi 2028.

Aidha, Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF) umeombwa kuboresha utendaji wake na kuimarisha uaandaaji na utekelezaji wa miradi. Uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi kwa nchi zinazoendelea unapaswa kuzingatiwa katika shughuli za GEF na umetakiwa kuendelea kujenga uwezo wa nchi zinazoendelea kupitia programu yake ya Capacity Building Initiative (CBI) na kusaidia nchi zinazoendelea katika utekelezaji wa Mipango ya Taifa ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi.

GCF imetakiwa kuendelea kutoa msaada wa fedha kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza Mipango ya taifa ya Kuhimili Mabdiliko ya Tabianchi na Bodi ya GCF imetakiwa kuendelea kutoa ithibati na kusajili taasisi za kitaifa na kikanda zitakazowezesha upatikanaji wa fedha kupitia taasisi hizo kwa mujibu wa taratibu za GCF. Kipaumbele kitakuwa kwa nchi na kanda ambazo hazina kabisa au zina taasisi chache ambazo tayari zimepata usajili kwenye mfuko wa GCF.

### Lengo la pamoja la kukusanya fedha za mabadiliko ya tabianchi

Mjadala ulihusu kuweka malengo mapya ya kukusanya fedha za kushughulikia mabadiliko ya tabianchi kwa kuzingatia mahitaji ya nchi zinazoendelea. Hatua hii inatokana na sababu kuwa malengo ya kukusanya Dola za Marekani 100 Bilioni yaliwekwa bila kuzingatia mahitaji na hali halisi ya nchi zinazoendelea. Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund -GCF) umepokea ahadi ya fedha zaidi wakati wa COP na kuwezesha kufikia Dola za Marekani 12.8 billion katika awamu ya pili.

Uamuzi uliofikiwa ni kuwa Mkutano umetambua uwepo wa pengo kubwa katika utoaji wa fedha. Kiasi cha Dola za Marekani 5.8-5.9 Trilioni zinahitajika kwa mwaka ili kufikia malengo ya upunguzaji wa uzalishaji wa gesi joto ifikapo mwaka 2030.

Nchi wanachama wamekubaliana kuweka mikakati ya kuanza kukusanya kiasi cha Dola Marekani 215 -387 Bilioni kwa mwaka; kuvutia uwekezaji katika eneo la nishati safi ambapo kiasi cha Dola za Marekani 4.7 hadi 5.00 trilioni kinahitajika kila mwaka hadi mwaka 2030; kuongeza ushiriki wa sekta binafsi na nchi zilizoendelea kuendelea kutoa fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

### Kilimo na Mabadiliko ya Tabianchi

Majadiliano ya ajenda ya Kilimo yalijikita katika kufanya mapitio ya mpango kazi wa kilimo na mabadiliko ya tabianchi ujulikanao kama (Koronivia Joint Work on agriculture - KJWA) ambao unajumuisha maeneo ya kilimo na usalama wa chakula na athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya kilimo. Aidha, majadiliano yalihusu migogoro na usalama wa chakula duniani na jinsi ya kukabiliana nayo.

Uamuzi Uliofikiwa ni kuwa Nchi zimeombwa kuongeza jitihada na msaada katika kujenga uwezo wa nchi na uendelezaji na uhaulishaji wa teknolojia ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuongeza uhimilivu wa wakulima na sekta za kilimo dhidi ya athari hizo.

Aidha, nchi na taasisi za kimataifa zimeombwa kuongeza na kuimarisha shughuli za kilimo kwa kushirikisha makundi mbalimbali ikiwemo vijana, wanawake na jamiii ili kupambana na janga la njaa na kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula duniani.

Nchi zimekubaliana na kusaini azimio la Pamoja kuhusu masuala ya mfumo wa kilimo na chakula kwa lengo kuimarisha mchango wa sekta hii katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.









**Limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Ofisi ya Makamu wa Rais**
S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 266 235 2038 • Nukushi +266 235 0002
Barua pepe: km@vpo.go.tz • Tovuti: www.vpo.go.tz
Ofisi ya Makamu wa Rais blog.vpo.go.tz